

More past papers are available on <http://www.kenyaplex.com>

Kenya Methodist University Sarufi na Matumizi ya Lugha I (KISW 001) Past Paper

MUDA: SAA MBILI

Maagizo:

Jibu maswali yote.

Swali la Kwanza

Onyesha vitenzi katika sentensi hii

(al. 2)

Kuimba kwake kulivutia watazamaji.

Tambua aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo.

Chakula chake kimeliwa chote

(al. 2)

Mwanafunzi hodari ametuzwa zawadi tatu

(al. 2)

Swali la Pili

Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani?

(al. 3)

Mwizi

Kiwete

Nguo

Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu.

(al. 3)

Pale ndiko alimoingia nyoka.

Andika kwa wingi.

(al. 2)

Mtoto aliyepotea jana amepatikana

Gari lake limeanguka.

Swali la Tatu

Kanusha

(al. 2)

Nimekula chakula

Alicheza mpira na akatuzwa

Tunga sentensi sahihi kuonyesha matumizi ya alama zifuatazo za uakifishaji.

(al. 3)

?

.

:

Swali la Nne

Eleza maana tofauti kati ya sentensi zifuatazo.

(al. 4)

Alikula chakula chote

Alikula chakula chochote

Tumia 'O' rejeshi katika sentensi hii.

(al. 2)

Shamba ambalo limalimwa ni letu.

Andika kwa udogo.

(al. 1)

Mtoto anayelia ni wangu.

Swali la Tano

Andika sentensi ukitumia neno 'kulima' kama nomino na kisha kama kitenzi.

(al. 2)

Tunga sentensi ukitumia kinyume cha neno lifuatalo oa_____

(al. 2)

Jaza mapengo kwa kutumia vivumishi vya pekee.

(al. 5)

Mwanafunzi _____ ni mkarimu sana.

Itabidi usafishe pahali _____

Jitu _____ kuwahangaisha watu limeuwawa.

Ameyamwaga maji _____

Uzalendo _____ unashangaza.

Geuza sentensi ulizokamilisha katika swali la (b) katika hali ya wingi.

(al. 5)

Swali la Sita

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kitenzi ulichopewa kwenye mabano.

(al. 5)

Ndizi ya nyanya _____ (iva)

Uteo wa mama _____ (toboka)

Kuzurura kwake _____ (udhi)

Barua ya kirafiki _____ (andika)

Mche _____ (chomoka)

Swali la Saba

Tunga sentensi ukitumia viunganishi vifuatavyo.(al 5)

Na

Lakini

Licha

Ila

Mpaka

Swali la Nane

Tunga sentensi ukitumia maneno uliyopewa ukizingatia hali zilizo katika mabano.(al. 10)

Chora (tendewa)

Pika (tendeka)

Andika (tendesha)

Salimu (tendeanana)

Bomoa (tendatenda)